# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**16 APRILI 2026**

*Hupigwa Chapa kwa Idhini ya Serikali na Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* — *Hutolewa kila Ijumaa*

*Bei Tshs . 3000/=* — **CXXXV Nam. 7494**


**YALIYOMO** *Ukurasa*


Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na kutunga upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa madhumuni ya kuendesha Biashara ya Magazeti na kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo..............................742


**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

---

**TANGAZO**

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 6 Mei, 2026 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
**16 Aprili, 2026**

(Ndugu Saleh Juma Mussa)
***Kaimu Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.***


**Matangazo yaliyohusu Waliofariki na Mali wa Watu waliofariki, kuvunja Mikataba ya ushirikiano, taarifa za Makampuni, Upotevu na marekebisho ya Nyaraka za Serikali na mengineyo ambayo ni muhimu kwa Umma lazima kuchapishwa katika Gazeti Rasmi. Nakala za Matangazo hayo zipelekwe kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania SLP 261 Maruhubi, Zanzibar. Nakala ziwasilishwe kabla ya Siku ya Alhanisi ya kila Wiki**

**MSWADA**

*wa*

**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUANZISHA SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI, NAM. 11 YA 2008 NA KUTUNGA UPYA SHERIA YA SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR KWA MADHUMUNI YA KUENDESHA BIASHARA YA MAGAZETI NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar, 2026 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7(1) cha Sheria hii;

"Magazeti ya Shirika" maana yake ni magazeti yaliyoanzishwa chini ya kifungu cha 17(1) cha Sheria hii;

"gazeti" maana yake ni aina ya maudhui inayoandaliwa na kuchapishwa au kutolewa mtandaoni na Shirika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na yaliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria husika na inajumuisha jarida;

"habari" maana yake ni taarifa kuhusu matukio ya karibuni yanayotokea ndani au nje ya nchi au ndani ya eneo maalumu la shughuli;

"Mhariri Mwendeshaji" maana yake ni Mhariri Mwendeshaji wa Shirika aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 13(1) cha Sheria hii;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Bodi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 7(1) (a) cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Shirika"maana yake ni Shirika la Magazeti Zanzibar lililoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii; na

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya habari.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA SHIRIKA

**3.**-(1) Kunaanzishwa Shirika litakalojulikana kama Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar. Kuanzishwa kwa Shirika.

(2) Shirika litakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri na kwa jina lake, kwa mujibu wa sheria husika, kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushitaki na kushitakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuondoa mali inayohamishika na isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(d) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi ya fedha yoyote; na

(e) kutekeleza au kufanya jambo lolote ambalo Shirika kwa asili yake linaweza kulitekeleza kwa mujibu wa sheria.

**4.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Shirika katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi. Muhuri na nembo ya Shirika.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo katika waraka wowote wa Shirika yatathibitishwa kwa saini ya Mhariri Mwendeshaji au afisa mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Mhariri Mwendeshaji.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Shirika utawekwa muhuri wa Shirika na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

. **5.** Malengo ya Shirika yatakuwa ni: Malengo ya Shirika.

(a) kuwa kituo cha biashara ya huduma za habari na biashara zinazolingana;

(b) kuwa kituo cha maudhui bora yanayojumuisha habari za uchunguzi na zenye maslahi ya umma; na

(c) kuwa kiungo baina ya Serikali na umma.

**6.** Kazi za Shirika ni: Kazi za Shirika.

(a) kuchapisha na kusambaza magazeti;

(b) kuchapisha matangazo na makala;

(c) kufanya biashara ya vifaa vya ofisini na vifaa na huduma za uchapaji;

(d) kutangaza na kusambaza sera na mikakati ya Serikali; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote inayohusiana na au muhimu kwa ajili ya kutekeleza masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SHIRIKA

Uanzishwaji na muundo wa Bodi.

**7.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mhariri Mwendeshaji;

(c) Mkurugenzi anayehusika na huduma za habari;

(d) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(e) mwakilishi kutoka Jumuiya ya Wanahabari mwenye taaluma ya uandishi wa habari, mawasiliano ya umma au fani nyengine yoyote inayohusiana na uandishi wa habari;

(f) mwakilishi kutoka Jumuiya ya Kitaifa ya Wafanyabiashara Zanzibar ambaye ni mtaalamu wa uchumi, fedha, biashara au fani nyengine yoyote inayofanana nazo; na

(g) mtu mwenye uzoefu katika huduma za uchapaji.

(2) Wajumbe chini ya aya ya (d), (e), (f) na (g) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na wakuu wa taasisi husika kwa kuzingatia sifa, uzoefu na jinsia zao.

Sifa za Mwenyekiti.

**8.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani yoyote inayohusiana na vyombo vya habari au biashara kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba katika huduma au biashara ya habari; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Bodi.

**9.** Kazi za Bodi ni:

(a) kusimamia masuala yanayohusu usimamizi wa Shirika na utekelezaji wa kazi zake;

(b) kutoa miongozo ya kimkakati kwa Shirika;

(c) kumshauri Waziri juu ya masuala ya Shirika;

(d) kusimamia utekelezaji wa sera za Shirika;

(e) kuidhinisha fedha, rasilimali na uwekezaji unaofanywa na Shirika; na

(f) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo inaweza kuwa ni muhimu kwa ajili ya kufikia malengo ya Shirika.

.

**10.** Bodi itakuwa na uwezo wa: Uwezo wa Bodi.

(a) kumuelekeza Mhariri Mwendeshaji kuipatia taarifa yoyote, ripoti au waraka mwengine ambao Bodi itaona ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake;

(b) kuidhinisha:

(i) bajeti, mpango kazi na sera za Shirika;

(ii) Kanuni za Wafanyakazi na Kanuni za Fedha;

(iii) ada na tozo kwa ajili ya huduma zinazotolewa na Shirika;

(c) kupendekeza muundo wa utumishi wa Shirika;

(d) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Shirika;

(e) kuajiri wafanyakazi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

**11.** Masharti kuhusiana na mwenendo wa vikao vya Bodi yatakuwa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Sheria hii. Mwenendo wa vikao vya Bodi.

**12.**-(1) Bodi itateua afisa wa Shirika kuwa Katibu wa Bodi. Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza ya fani ya sheria au mwenye sifa ya Katibu wa Shirika kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali; na

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na:

(a) kwa kushauriana na Mwenyekiti, ataandaa ajenda za vikao vya Bodi;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza kumbukumbu sahihi na zinazojitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(e) atatekeleza jukumu jengine lolote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

**13.**-(1) Kutakuwa na Mhariri Mwendeshaji wa Shirika ambaye atateuliwa na Rais. Uteuzi wa Mhariri Mwendeshaji.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mhariri Mwendeshaji ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya habari, mawasiliano ya umma, uandishi wa habari au fani inayolingana nazo kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi ya habari kwa kipindi kisichopungua miaka saba; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mhariri Mwendeshaji.

**14.**-(1) Mhariri Mwendeshaji atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Shirika na atakuwa na wajibu wa kusimamia kazi za kila siku za Shirika.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mhariri Mwendeshaji:

(a) atawajibika kwa mapato yote, matumizi na mali za Shirika;

(b) atahakikisha wafanyakazi wa Shirika wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili na uwajibikaji;

(c) atasimamia masuala ya nidhamu kwa wafanyakazi wa Shirika; na

(d) atatekeleza jukumu jengine lolote kama Bodi inavyoweza kuelekeza.

Idara, vitengo na divisheni.

**15.**-(1) Shirika litaanzisha idara, vitengo na divisheni kwa idadi na namna kama itakavyokuwa muhimu katika kutekeleza kazi za Shirika.

(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Bodi kutokana na mapendekezo ya Mhariri Mwendeshaji.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mhariri Mwendeshaji na kuthibitishwa na Bodi kulingana na sifa zao.

(4) Wakuu wa idara, divisheni na vitengo watawajibika kwa Mhariri Mwendeshaji.

Wafanyakazi wa Shirika.

**16.** Kutakuwa na wafanyakazi wa Shirika watakaoajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

## SEHEMU YA NNE
## KUANZISHWA KWA MAGAZETI YA SHIRIKA

Magazeti ya Shirika.

**17.**-(1) Kutakuwa na magazeti ya Shirika ambayo yatasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

(2) Magazeti ya Shirika chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki yatajumuisha:

(a) Gazeti la Zanzibar Leo;

(b) Gazeti la Zanzibar Mail;

(c) Gazeti la Zaspoti; na

(d) gazeti jengine lolote ambalo Shirika linaweza kuanzisha.

(3) Mhariri Mwendeshaji anaweza, kwa kuzingatia idhini ya Bodi, kuanzisha au kubadilisha mpangilio au muonekano wa magazeti kulingana na mahitaji ya soko.

Sera ya Biashara na Uhariri wa Shirika.

**18.**-(1) Shirika litakuwa na sera ya biashara na miongozo ambayo inaainisha huduma za uchapaji, uuzaji wa magazeti, vifaa vya ofisi na kuandikia, matangazo au biashara nyengine yoyote ya Shirika.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Shirika litaanzisha sera yake ya uhariri kwa ajili ya kudhibiti maudhui ambayo itazingatia kanuni za maadili, misingi na viwango vya habari.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Shirika halitochapisha au kukata kuchapisha maudhui yoyote kwa misingi ya vitisho au ushawishi kutoka kwa mtu yeyote.

Uuzaji na usambazaji wa magazeti.

**19.**-(1) Shirika litaanzisha mfumo wa kuuza na kusambaza magazeti utakaowafikia wateja kwa sehemu kubwa ndani na nje ya Tanzania.

(2) Shirika linaweza, mbali na mfumo wa kusambaza magazeti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kuanzisha usambazaji wa magazeti kwa njia ya mtandao.

Biashara ya vifaa vya kuandikia na vifaa vya ofisi.

**20.** Shirika, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 6 cha Sheria hii, litajihusisha na biashara ya vifaa vya kuandikia, vifaa vya ofisi na huduma za uchapaji.

Mtambo wa uchapaji.

**21.** Shirika linaweza kumiliki na kuendesha mtambo wake wa uchapaji kwa ajili ya kuchapisha magazeti na shughuli nyengine.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Shirika.

**22.** Fedha na rasilimali za Shirika zitajumuisha:

(a) kiwango cha fedha kitakachoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) ruzuku, zawadi, msaada, michango au mikopo kama Shirika litakavyopokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote;

(c) ada na tozo kutokana na huduma zinazotolewa na Shirika; na

(d) fedha nyengine yoyote ambayo inaweza kupatikana kihalali na Shirika.

Bajeti ya Shirika.

**23.**-(1) Mhariri Mwendeshaji, kila mwisho wa mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Bodi, kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa, makadirio ya mapato na matumizi ya Shirika kwa mwaka unaofuata wa fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Umma, Nam. 12 of 2016.

(2) Bodi, baada ya kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Shirika itawasilisha kwa Waziri.

Hesabu na ukaguzi.

**24.**-(1) Shirika litaweka na kutunza kwa usahihi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Mhariri Mwendeshaji, katika kila mwaka wa fedha, ataandaa au ataagiza kuandaliwa:

(a) taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za mwaka wa fedha husika;

(b) taarifa ya mali na madeni ya Shirika hadi kufikia siku ya mwisho ya mwaka wa fedha kwa ajili ya kuwasilishwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi mwingine yeyote aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(c) taarifa nyengine yoyote ya fedha kama ilivyoelezwa na sheria.

Ufunguaji wa hesabu za benki.

**25.** Shirika litafungua hesabu ya benki kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Kutangaza shughuli za Serikali kwenye gazeti.

**26.**-(1) Taasisi zote za Serikali zitatakiwa kuchapisha matangazo yao kuhusu shughuli za taasisi zao katika magazeti ya Shirika.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, taasisi za Serikali zinaweza kutoa tangazo lake katika gazeti jengine lolote.

(3) Shirika litatayarisha muongozo kuhusu matangazo kutoka kwa taasisi za umma.

Wajibu wa Shirika kwa Jamii.

**27.** Shirika, kwa kuzingatia sheria husika, litaandaa mkakati wa Uwajibikaji kwa Jamii kwa mujibu wa biashara zao.

Kanuni.

**28.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**29.**-(1) Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote halali lililofanywa chini ya sheria iliyofutwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litachukuliwa kuwa limefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

## JADWELI

## MWENENDO WA VIKAO VYA BODI
**[Chini ya kifungu cha 11]**

Makamu Mwenyekiti.

**1.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Muda wa wajumbe.

**2.** Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

**3.**-(1) Bodi itakutana kikawaida kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana muda wowote itakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti na ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**4.** Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wataunda akidi katika kikao chochote cha Bodi.

Uamuzi wa Bodi.

**5.** Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa maafikiano, endapo hakuna maafikiano, uamuzi utafanywa kwa kupiga kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za vikao.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kujipangia taratibu zake wenyewe kuhusiana na vikao na uendeshaji mzuri wa shughuli zake.

Mjumbe mualikwa.

**7.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye sio mjumbe wa Bodi kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kamati za Bodi.

**8.** Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalumu kama itakavyoona inafaa.

Kumbukumbu za vikao vya Bodi.

**9.** Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu.

Kukasimu kazi za Bodi.

**10.**-(1) Bodi inaweza, itakavyoona inafaa kwa ajili ya kutekelezaji wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati za Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji bora za kazi.

Kubainisha maslahi.

**11.** -(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kuzingatiwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya uamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

**12.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyomteua mjumbe huyo;

(e) ikiwa atasimamishwa na Waziri akishindwa kutimiza matarajio ya Mamlaka; au

(f) amefariki.

Posho la wajumbe wa Bodi.

**13.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watasitahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti Zanzibar, Nam. 11 ya 2008 na kutunga upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa ajili ya kuweka masharti yanayohusiana na uendeshaji na usimamizi wa Shirika.

Kwa ujumla, Mswada huu unalenga kuimarisha utendaji kazi wa Shirika kwa kulipa hadhi ya kisheria inayokidhi mahitaji ya sasa, na kuweka mfumo madhubuti wa uendeshaji wa shughuli zake. Aidha, Mswada unaweka masharti yatakayoliwezesha Shirika kufanya shughuli za kibiashara, ikiwemo kumiliki na kuendesha mitambo ya uchapishaji, ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa magazeti na maudhui mengine.

Vilevile, Mswada unakusudia kuhakikisha kuwa Shirika linazalisha na kusambaza maudhui yenye ubora, yanayozingatia maadili na viwango vya taaluma ya uandishi wa habari, na hivyo kulifanya Shirika liweze kujitegemea kiuchumi na kiutendaji.

Mswada huu umegawika katika sehemu sita kama ifuatavyo:

***Sehemu ya Kwanza:*** Sehemu hii inaweka masharti ya awali ambayo yamejumuisha jina fupi na kuanza kutumika na ufafanuzi wa baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika katika Mswada huu.

***Sehemu ya Pili:*** Inaelezea uanzishwaji wa Shirika, muhuri na nembo, malengo na kazi za Shirika.

***Sehemu ya Tatu:*** Sehemu hii inahusu usimamizi na uendeshaji wa Shirika, Uanzishwaji wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Magazeti, Katibu wa Bodi, kazi na uwezo wa Bodi, uteuzi wa Mhariri Mwendeshaji, kazi za Mhariri Mwendeshaji, Uanzishwaji wa idara, vitengo na divisheni ili kuhakikisha Shirika linatekeleza kazi zake kwa weledi, ufanisi na kwa wakati pamoja na uajiri wa wafanyakazi wa Shirika.

***Sehemu ya Nne:*** Sehemu hii inaelezea kuhusu uanzishwaji wa Magazeti ya Shirika, Sera ya Biashara na Uhariri, uuzaji na usambazaji magazeti, biashara ya vifaa vya kuandikia na umiliki na uendeshaji wa mtambo wa uchapaji.

***Sehemu Tano:*** inahusu masharti ya fedha, vyanzo vya fedha za Shirika, bajeti ya Shirika, ukaguzi na uwezo wa Shirika kufungua akaunti ya benki.

***Sehemu ya Sita:*** inaelezea kuhusu masharti mengineyo ambayo yanajumuisha masharti ya kutangaza shughuli za serikali kwenye gazeti, wajibu wa Shirika kwa jamii, uwezo wa Waziri kutunga kanuni na kufutwa kwa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na kubakiza.

Mwisho, lipo Jadweli linaloeleza masharti kuhusu mwenendo wa vikao vya Bodi.



ZANZIBAR ( MHE.DKT. RIZIKI PEMBE JUMA)
**16 Aprili, 2026** **WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

*LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR 2026*